

## Je, wewe umejiandaa kwa janga?

Matukio makali ya hali ya hewa yanaweza kutokea wakati wowote wa mwaka huko Queensland na yanaweza kukuathiri wewe na familia yako na kuharibu mali. Matukio haya yanaweza kujumuisha dhoruba kali, mafuriko, tufani, tetemeko la dunia au moto wa misitu.

Hatuwezi kudhibiti hali ya hewa, lakini tunaweza kujiandaa.

Kabla ya janga, angalia kama una:

- ✓ mpango wa dharura kwa wewe na familia yako, ikijumuisha mpango kwa wanyama wako
- ✓ orodha ya watu kuwasiliana nao katika dharura
- ✓ bima ya kisasa
- ✓ umeandaa begi la vitu muhimu vya kuchukua nawe wakati wa dharura.

Ili kupata habari na vidokezo zaidi kuhusu kuandaa kwa janga, tembelea kwa [www.getready.qld.gov.au](http://www.getready.qld.gov.au)

## Kupata wapi msaada baada ya maafa

**Usaidizi wa kihisia na wa vitendo unapatikana kutoka mashirika ya serikali na yasiyo ya faida kwa ajili ya watu walioathiriwa na maafa.**

## Usaidizi wa kibinafsi na ushauri nasaha

Ni kawaida kupata hisia nyingi baada ya maafa. Usaidizi wa kibinafsi na wa vitendo unapatikana ikiwa unapata mkazo wa kihisia au unatatiza kuvumilia.

Tafuta usaidizi ikiwa wewe, mwanafamilia au rafiki:

- akipata mkazo wa kihisia au kisaikolojia
- akihisi uchovu, kukasirika au kutambua mabadiliko katika mifumo ya hamu yako ya kula au ya kulala
- akitambua mabadiliko ya tabia kama vile matumizi yaliongezeka ya pombe au dawa zingine za kulevya au kujiondoa kutoka dawa nyingine
- akihitaji mtu tu kuongea naye.

## Habari ya mawasiliano ya usaidizi wa kibinafsi na ya ushauri nasaha

- Lifeline Australia (ushauri nasaha) – **13 11 14**
- Shirika la Msalaba Mwekundu la Australia (Australian Red Cross) – **1800 733 111**
- St. Vincent de Paul – **13 18 12**
- Queensland Health – **13 HEALTH (13 43 25 84)**
- Msaada wa Makazi (Housing Assistance) – **13 QGOV (13 74 68)**
- Huduma ya Dharura ya Jimbo (State Emergency Service) (SES) – **13 25 00**
- Simu ya Haraka ya Kupona kwa Jamii – **1800 173 349**

Ili kupata habari za mawasiliano za huduma za usaidizi za jamii za mtaa na za jumla zinazopatikana katika eneo lako, tembelea [www.qld.gov.au/disasterhelp](http://www.qld.gov.au/disasterhelp) na tafuta 'regional community support'.

## Usaidizi wa kifedha

**Usaidizi wa kifedha na huduma za msaada huenda kupatikana ikiwa umeathiriwa na janga.**

Usaidizi hutolewa kupitia Mipango ya Ufadhili wa Kupona Majanga ya Jumuiya ya Madola na Jimbo inayofadhiliwa kwa pamoja (DRFA).

## Ruzuku\*

- ✔ **Msaada wa Magumu ya Dharura** – kwa watu katika maeneo yaliyotangazwa yenye maafa ili kusaidia mahitaji ya haraka na ya muhimu kama vile chakula, mavazi na dawa.
- ✔ **Ruzuku ya Yaliyomo Muhimu ya Kaya** – ni kusaidia watu katika maeneo yaliyotangazwa yenye maafa ambao hawana bima au hawezi kudai bima ya kuchukua nafasi ya yaliyomo muhimu ya kaya.
- ✔ **Ruzuku ya Usalama na Uunganisho Tena wa Huduma Muhimu** – kwa watu katika maeneo yaliyotangazwa yenye maafa ili kusaidia kuunganisha tena huduma muhimu kama vile umeme, gesi, maji, mifumo ya maji taka au maji machafu.
- ✔ **Ruzuku ya Msaada wa Magumu ya Huduma Muhimu** – husaidia watu walioathirika moja kwa moja na janga ili kukidhi mahitaji ya haraka wakati huduma muhimu moja au zaidi inapokatika kwa zaidi ya siku tano.
- ✔ **Ruzuku ya Msaada wa Kimuundo** – kwa watu katika maeneo yaliyotangazwa yenye maafa ili kusaidia kutengeneza nyumba zao na kufanya nyumba kuwa thabiti na salama kuishi.

\*Vigezo vya kustahiki vinatumika

Ili kujua ni ruzuku zipi zinazopatikana katika eneo lako na kuangalia kustahiki kwako, tembelea [www.qld.gov.au/disasterhelp](http://www.qld.gov.au/disasterhelp)

## Maelezo zaidi

Serikali ya Queensland hutoa huduma za wakalimani ili kutoa habari kuhusu maafa, ruzuku au usaidizi katika lugha yako.

Piga simu kwa **1800 512 451** na uliza kwa mkalimani katika lugha unayopendelea au piga simu kwa Simu ya Haraka ya Kupona Jamii kwa **1800 173 349**.

